**KATIKA MAHAKAMA KUU YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**DIVISHENI YA KAZI**

**ILIYOKAA DAR ES SALAAM**

**SHAURI LA MAREJEO NA. 31 LA 2020**

**KATI YA**

**SAMSON DEOGRATIUS SHEMBUSHO....................................MLETA MAOMBI**

**NA**

**CHINA RAILWAY SEVENTH GROUP (CRSG)...........................MJIBU MAOMBI**

**HUKUMU**

Tarehe ya Amri Ya Mwisho: 08/03/2021
Tarehe ya Hukumu: 11/06/2021

**A. E. MWIPOPO, J.**

Shauri hili la marejeo limefunguliwa dhidi ya Uamuzi wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi katika Mgogoro wa Kazi Na. CMA/DSM/TEM/245/2019/119/2019. Samson Deogratius Shembusho ambaye ni mleta maombi anaomba Mahakama itoe amri zifuatazo:-

1. Kwamba Mahakama iitishe na kurekebisha tuzo ya Tume ya Usuluhishi na Uamuzi iliyotolewa tarehe 23 Disemba, 2019 na Mhe. H. Amos, Mwamuzi, katika Mgogoro wa Kazi Na. CMA/DSM/TEM/245/2019/119/2019 na kuiweka pembeni (set aside) tuzo hiyo na kutoa amri nyingine muhimu kutokana na maombi yaliyotolewa katika Wito wa Chemba (Chamber Summons).

2. Na nafuu nyingine yoyote Mahakama itaona kuwa inafaa na ya haki (just).

Shauri hili limeungwa mkono na kiapo cha Mleta Maombi ambacho katika aya ya 11 kuna hoja mbili za kisheria (legal issues) zinazotokana na ushahidi. Hoja hizo ni kama zifuatazo:-

i. Kwamba mgogoro uliokuwa mbele ya Tume haukushughulikiwa vizuri kiutaratibu kwa kuwa wakati wa usikilizwaji Mjibu Maombi hakutoa ushahidi na alishindwa kuthibitisha kuwa Mleta Maombi alikataa kurejea kufanya kazi.

ii. Kwamba ilikuwa ni kosa kiushahidi na kisheria kuamua kuwa Mleta Maombi hakuachishwa kazi wakati hakuna ushahidi uliowasilishwa na Mjibu Maombi kuonesha kuwa uachishwaji kazi ulikuwa halali au Mleta Maombi hakuwa ameachishwa kazi.

Historia fupi ya shauri hili ni kwamba Mleta Maombi aliajiliwa na Mjibu Maombi aitwaye China Railway Seventh Group (CRSG) kama Msimamizi (foreman) tarehe 13 Julai, 2018. Inadaiwa tarehe 26 Januari, 2019 alifukuzwa kazi. Mleta Maombi alipeleka malalamiko yake mbele ya Tume ambayo katika uamuzi wake ilikubaliana na Mjibu Maombi kuwa Mleta Maombi hakuachishwa kazi. Mleta Maombi hakuridhika na Uamuzi huo wa Tume ndipo akafungua shauri hili hapa Mahakamani.

Shauri hili lilisikilizwa upande mmoja (exparte) kufuatia kitendo cha Mjibu Maombi kuthibitika kupokea wito wa kufika mbele ya Mahakama mara kadhaa lakini hakuwahi kufika kusikiliza shauri lake. Hivyo mnamo tarehe 14 Aprili, 2021, baada ya Mleta Maombi kuthibitisha kumpatia Mjibu Maombi wito wa kufika Mahakamani kwa tarehe hiyo ambapo hakufika, Mleta Maombi aliomba shauri lisikilizwe bila Kuwepo kwa Mjibu Maombi na lisikilizwe kwa Maandishi maombi ambayo yalikubaliwa na Mahakama. Mleta Maombi katika shauri hili alikuwa anawakilishwa na Bi. Tukelage Frank, Wakili wa Kujitegemea.

Wakili wa Mleta Maombi akitoa Mawasilisho (Submission) kuunga mkono shauri hili alieleza kuwa Mleta Maombi alikuwa na mkataba wa ajira wa kudumu na Mjibu Maombi. Alieleza kuwa anazo sababu nne za kuomba marejeo haya. Aleleza kuwa sababu yake ya kwanza ni kuwa Mwamuzi alishindwa kuona kuwa Mleta Maombi aliachishwa kazi isivyo halali na Mjibu Maombi. Ameeleza kuwa Mleta Maombi hakujiachisha kazi kama ilivyoamuliwa na Tume ambayo iliona kielelezo D1 – Makubaliano ya Kumaliza Mgogoro kinaonesha kuwa Mleta Maombi aliacha kazi. Ameeleza kilelezo D1 kinaonesha kuwa Mleta Maombi anakubali kulipwa shilingi 625,000/= kama fidia ya kusimamishwa kazi na sio malipo ya kuachishwa kazi. Hivyo ilibidi Mjibu Maombi akae na Mleta Maombi kwa ajili ya malipo ya kuachishwa kazi.

Wakili anaeleza kuwa ushahidi wa Mleta Maombi unaonesha kuwa aliachishwa kazi tarehe 20 Januari, 2019 na sababu ni kuwa hakuna kazi ya kufanya. Ila tarehe zilizofuata kulifanyika hatua za kuokoa hali hiyo. Tarehe 8 Mei, 2019 ilikuwa ni tarehe ya kikao cha mwisho cha usuluhishi. Kielelezo D1 hakikuwa halali kwa sababu Mleta Maombi alisimamishwa kazi bila akilipwa nusu mshahara na pia hakuambiwa kosa lake. Hivyo kusimamishwa huko hakukuwa halali kama ilivyoamuliwa na Mahakama hii katika kesi ya **Chai Bora Limited** dhidi ya **Allan Telly Mtukula, Marejeo Na. 38 ya 2018, Mahakama Kuu, Divisheni ya Kazi, iliyoketi Arusha**.

Wakili wa Mleta Maombi alieleza kuwa sababu yake ya pili ya marejeo ni kuwa Mwamuzi alikosea kisheria na kiushahidi kwa kujizuia kuchambua makosa ya msingi ya kisheria. Makosa hayo ni kuwa Mleta Maombia aliachishwa kazi tarehe 20 Januari, 2019 bila kufuata sera na taratibu zake zinazoongoza masuala ya kinidhamu. Aidha, kanuni ya 27(2) ya Kanuni za Ajira na Mahusiano Kazini (Kanuni za Utendaji Bora), Tangazo la Serikali Na. 42 la 2007 inaeleza kuwa mwajiriwa atasimamishwa kazi huku akilipwa mshahara wake kamili.

Kuhusu sababu ya tatu, Wakili wa Mleta Maombi alieleza kuwa Mwamuzi alikosea kwa kushindwa kuchambua uhalali wa sababu za kumwachishwa kazi Mleta Maombi. Ameeleza kuwa Mjibu Maombi hakutoa

ushahidi kabisa bele ya Tume kuonesha taratibu alizofuata katika kumwachisha kazi Mleta Maombi. Na jambo hilo ni kinyume na kifungu cha 37(2) (c) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura ya 366 ya Sheria kama Ilivyorejewa Mwaka 2019.

Na mwisho, Wakili wa Mleta Maombi aliomba Mahakama impatie Mleta Maombi fidia ya mshahara wa miezi 12 kutokana na kuachishwa kazi isivyo halali pamoja na mshahara wa mwezi mmoja kama taarifa ya kuachishwa kazi.

Kutokana na mawasilisho hayo, nimeona kuwa kuna hoja tatu ambazo Mahakama hii inabidi izifanyie uamuzi. Hoja hizo ni kama zifuatazo:-

1. Endapo Mleta Maombi aliachishwa kazi na Mjibu Maombi.
2. Kama jibu katika hoja ya kwanza ni chanya, iwapo uachishwaji kazi huo ulikuwa halali.
3. Na ipi nafuu inayostahili kwa kila upande.

Katika kuamua hoja ya kwanza niliona kuna umuhimu wa kuangalia kanuni ya 3 ya Kanuni za Ajira na Mahusiano Kazini (Kanuni za Utendaji Bora), Tangazo la Serikali Na. 42 la 2007. Kanuni hiyo inaonesha aina mbalimbali za uachishaji kazi. Uachishaji kazi huo ni pamoja na kuachishwa kazi kwa sheria ya kimila ya Uingereza (Common Law). Kanuni hizo zinaeleza katika kanuni ya 3(2) kuwa kuachisha kazi kihalali chini ya sheria

Labour Court Tz.

ya kimila ya Uingereza ni pamoja na kuachishwa kazi kwa makubaliano, ajira kukoma yenyewe, kuachishwa kazi kunakofanywa na mwajiri au ukatishwaji wa ajira unaofanywa na mfanyakazi (resignation).

Katika shauri hili Mleta Maombi ameeleza kuwa Mwamuzi alikosea kuona kuwa hakuachishwa kazi na Mjibu Maombi wakati ushahidi unaonesha kuwa aliachishwa kazi siku ya tarehe 20 Januari, 2019. Nimepitia ushahidi uliomo katika rekodi za Tume, ushahidi huo unaonesha kuwa Mleta Maombi alikuwa ameajiriwa kwa mkataba wa kazi wa kudumu 13 Julai, 2018. Mleta Maombi akitoa ushahidi wake mbele ya Tume alieleza kuwa bosi wake alimwachisha kazi tarehe 20 Januari, 2019 kwa sababu hakukuwa na kazi kwa kipindi hicho. Alidai kuwa kuachishwa hakukuwa halali na alipoenda kudai mafao yake ya kuachishwa kazi alipewa asaini makubaliano ya kulipwa mshahara wa mwezi mmoja kama inavyoonekana katika kielelez D1.

Nimekisoma kielelezo D1 ambacho kina nyaraka mbili, nyaraka ya kwanza ni hati ya makubaliano ya tarehe 8 Mei, 2019 baina ya Mleta Maombi na Mjibu Maombi. Hati hiyo inaonesha kuwa Mjibu Maombi aliomba Mleta Maomba arudi kazini lakini alikataa na kuwa wamekubaliana alipwe mshahara wa mwezi mmoja shilingi 642,900/= kama fidia ya mgogoro huo. Nyaraka inaonesha Mgogoro uliopo ni wa kusimamishwa kazi bila kulipwa kwa miezi miwili na Mleta Maombi alieleza kutokuwa tayari kurudi kazini

kwa mazingira yaliyopo. Nyaraka ya pili ya kielelezo D1 ni barua ya Mleta Maombi kwa Mwajiri ya tarehe 8 Mei, 2019 akimtaarifu kuwa anakubali kuwa amepokea shilingi 642,900/= kama fidia ya kusimamishwa kazi kwa miezi miwili bila malipo ya mshahara. Nyaraka zote mbili zimesainiwa na Mleta Maombi. Kielelezo D1 kimetolewa kama ushahidi na pande zote mbili. Hii inathibitisha kuwa ni nyaraka ambayo wote wanakubaliana na kilichomo katika nyaraka hiyo.

Mleta Maombi ameeleza kuwa walichokubaliana katika hati ya makubaliano ambayo ni sehemu ya kielelezo D1 ilikuwa kulipwa fidia kutokana na kusimamishwa kazi bila malipo. Aidha, barua yake ya kuthibitisha kupokea malipo ambayo nayo ni sehemu ya kielelezo D1 inaonesha kuwa ni malipo ya kufidia miezi 2 ambayo alisimamishwa kazi bila malipo. Ni maoni yangu kuwa ushahidi huu unathibitisha kuwa Mleta Maombi hakuwa ameachishwa kazi kama alivyodai bali alisimamishwa kazi kama mashahidi DW1 na DW2 walivyotoa ushahidi wao mbele ya Tume. Aidha, nyaraka ya kwanza ya kilelezo D1 imeeleza kuwa Mleta Maombi hakuwa tayari kurudi kuendelea na kazi katika mazingira yaliyopo. Hivyo ni wazi kuwa Mleta Maombi hakuachishwa kazi. Kwa sababu hiyo, nakubaliana na Mwamuzi kuwa ushahidi uliopo unaonesha kuwa Mleta Maombi hakuachishwa kazi na Mjibu Maombi, bali aliamua kutorudi kazini. Hivyo majibu ya hoja ya kwanza ni hasi.

Kwa kuwa nimeona kuwa Mleta Maombi hakuachishwa kazi na Mjibu Maombi ni wazi kuwa hakuna uachishwaji kazi usio halali uliofanywa na Mjibu Maombi. Kwa sababu hiyo Mleta Maombi hastahili kulipwa fidia au mshahara wa mwezi badala ya taarifa ya kuachishwa kazi.

Hivyo, nimeona kuwa shauri hili la marejeo halina mashiko na linatupiliwa mbali (dismissed). Kwa kuwa hoja ya kwanza inamaliza shauri hili sitazitolea uamuzi hoja zilizobakia. Hakutakuwa na gharama za kesi.

**A. E. MWIPOPO**
**JAJI**
**11/06/2021**

Labour Court Tz.